# Nchini India Watu Wanapotaka Nyumba, Huzijenga: Jarida la Thelasini na Tatu (2022)



Maandamano ya Chama Cha Kikomunisti Cha India, Mei 10 Mwaka 2022 Huko Khila Warangal.

Wapendwa Marafiki,

Salamu kutoka dawati la Tricontinental: Institute for Social Research.

Yote yalianza kwa utafiti. Aprili 2022,wanachama wa Chama Cha Kikomunisti India (Cha Kimarx), ama CPI(M),walipokwenda mlango kwa mlango ndani ya mji wa Warangal katika Jimbo la Telangana. Chana kilikwishakuwa na uwewa tayari juu ya changamoto zinazoikabili jamii ile lakini kilitaka kukusanya taarifa sahihi kabla ya kuunda mpango-kazi. Timu Thelasini na Tano za watu watatu mpaka wanne za wanachama wa CPI(M) na wakereketwa wa chama walikwenda katika takribani nyumba 45,000 na kujifunza juu ya namna ambavyo wakaazi walikuwa wakiteseka kwa masuala mbalimbali kama vile kukosekana kwa pensheni na chakula cha ruzuku. Wengi walieleza hisia kali juu ya suala la kukosekana kwa makaazi ya kudumu, huku theluthi wakisema hawakuwa wamiliki wa nyumba na hawakuwa wakimudu kulipa kodi zao. Serikali ilikuwa imeahidi kujenga  nyumba za vyumba viwili vya kulala kwaajili ya watu masikini, lakini ahadi hizi zilipotea kama mvuke.  Kutokana na mfumuko wa bei uliotafuna vipato vyao kiduchu na ukosefu sugu wa ajira unaotokana na kuanguka kwa kiwanda cha bidi (sigara) kilichokuwepo eneo hilo,

watu waliokutana na wanachama hao chama cha kikomunisti walikuwa katika hali ya kuvurugwa.

Wengi miongoni mwa wanajamii walionyesha utayari wa kupigania hali bora ya maisha, hususani suala la kujengwa vibanda zaidi (gudisela poratam). Kwa maneno ya mkaazi mmoja, 'liwalo na liwe, hata kama tutapigwa na kuuawa tutaunga mkono mapambano haya'. CPI(M) iliunda kamati katika kata thelasini za Jakkaloddi, sehemu ya Warangal, na kuanza kuwaandaa watu kwa mapambano yaliyokuwa yakija. Kitovu cha mapambano kilikuwa ni ardhi ambayo serikali iliitwaa mwisho mwa miaka ya 70 kutoka kwa kabaila mzee, Moinudinn Khadir, kwa kutumia sheria ya 'Land Ceiling Act' ya India ya mwaka 1975.

Hata hivyo, badala ya kuigawa ardhi ile kwa wasiokuwa na ardhi , serikali iliwaondoa wakulima kwa sehemu na kuwapa ardhi viongozi wa chama tawala cha Telugu Desam mwaka 1989.




Sagar, katibu wa CPI(M) wa Ragasaipeta na kiongozi wa kamati ya mapambano ya Jakkalodi, akihutubia wajumbe katika kikao cha chama cha kampeni Jakkaloddi Juni 18, 2022.

Mei 25,2022,watu 8000 waliandamana kuelekea Shirika la Manispaa ya Warangal na kuwasilisha maombi 10000 ya kupatiwa makaazi ya umma. Watu hao walipokwenda kuyatwaa maeneo tupu, polisi waliwaambia kukaa mbali na kuwazuia kuingia katika eneo lile. Licha ya hili, Kamati ya Mapambano ya Jakkalodi, iliundwa na wale ambao waliitwaa ardhi, waliomudu kuratibu ujenzi wa nyumba 3,000 katika ardhi waliyoitwaa. Saa 9 alfajiri  20, polisi walifika na kuchoma nyumba/vibanda vingi wakati watu wakiwa bado wamelala ndani, na kuwapiga waliozitwaa ardhi

kwa kadiri walivyokuwa wakijitokeza kutoka katika maskani zao za muda. Watu mia nne walikamatwa. Siku iliyofuata maofisa wa mamlaka za mitaa waliweka bango lililosomeka: 'Eneo hili ni kwaajili ya ujenzi wa jengo la mahakama.'

Si ishara hii wala ukatili wa polisi uliomudu kuwazuia watu, ambao walirejea na kuendelea kutia kambi pale kwa siku sitini, G. Nagaiah, mjumbe wa sekretarieti ya Jimbo CPI(M), alimuarifu P. Ambedkar wa Tricontinental Research Services (India). Juni 26, walianza kujenga vibanda vipya 2,000. Polisi walijaribu kuwazuia kwa ubabe na vurugu, lakini watu walijibu mapigo na kuwalazimisha polisi kurudi nyuma. Kwa sasa kuna vibanda 4600 Kwa Jumla.



Wanawake wakibishana na polisi, ambao wanajaribu kuwaondoa kutoka eneo lililotwaliwa,22 Juni 2022.

Hatua zilizochukuliwa na CPI(M) zilitokana na kushindwa kwa serikali na dola kuondoa 'njaa' kali ya ardhi katika ukanda ule. Takwimu za hivi karibuni za serikali zinaonyesha kwamba, kati ya mwaka 2012 mpaka 2017 kumekuwa na upungufu wa nyumba milioni 18.8 kwa maeneo ya mijini pekee nchini India.Hata idadi hii si sahihi kwa sababu inachukua nyumba za hadhi ya chini katika maeneo yenye mmbanano kama nyumba zenye kukidhi. Novemba 2021 ,Benki ya Dunia ilitangaza juu ya vigezo vya makaazi yenye kukidhi (Adequate Housing Index), vilivyotupa picha halisi. Takwimu zao za kiwango cha upishano za makaazi zinaonyesha kuwa, nchini India, familia mbili kati ya tatu za tabaka la wafanyakazi/wavuja jasho zinaishi makaazi yaliyo chini ya kiwango. Vigezo vya vya makaazi bora vilitizamiwa kwa takwimu kutoka mataifa masikini 64 vilikuta upungufu wa nyumba milioni 268 katika nchi hizi, hali inayowaathiri watu bilioni 1.26.

Zaidi, robo ya hazina ya makaazi yaliyopo katika mataifa masikini ni makaazi duni na hayatoshi. Wakati mabilioni ya watu wakiwa hawana makaazi ulimwenguni ama wakiishi katika makaazi duni, na kukiwa hakuna mpango wa maana kushughulika tatizo hili, haitegemewi kuwa taifa lolote masikini litatimiza Lengo la kumi na moja la maendeleo endelevu la 'kuyafanya majiji na makaazi ya watu kuwa jumuishi, salama, stahimilivu na endelevu'.

Mapambano ya ardhi katika maeneo kama Jakkaloddi yanafanana na yale yanayoongozwa na Abahlali baseMjondolo, vuguvugu la watu waishio katika maeneo mchafukoge (shack dwellers) nchini Afrika Kusini, na vuguvugu la Landless Workers' Movement (MST) nchini Brazil. Kamatakamata na uhamishwaji kimabavu wa watu masikini kutoka kwa waliozitwaa ardhi umekuwa ukijitokeza mara kwa mara ulimwenguni kote. Mashambulizi yanayofanana yamekuwa yalirudiwa huko Guernica, Argentina, ambapo familia 1,900 waliondolewa mnamo tarehe 29 octoba mwaka 2020, na huko Otodo-Gbame, Nigeria ambapo zaidi ya watu 30,000 waliondolewa kati ya Novemba 2016 na Aprili 2017.

Mapambano hayo yanaongozwa na watu ambao wanataka kukidhi mahitaji ya msingi ya kuishi katika staha.

Katika dozia yetu ya hivi karibuni mwenzetu kutoka Afrika Kusini Yvonne Phyllis alitumia lugha ya kiXhosa akisema kumaanisha ardhi:*umhlaba wookhokho bethu*, 'ardhi ya wazee wetu'. Kauli hii, ni ya kawaida mno katika tamaduni nyingi, ikichagiza kuwa ardhi itizamwe kama urithi wa pamoja na si mali ya mtu mmoja. Uelewa huu unachagiza kama ambavyo Phyllis anavyofafanua, kutambua juu ya 'swali ambalo halijapatiwa jawabu kuhusu kutokuwepo haki' lililorithiwa kutoka katika 'mchakato wa uporaji na ulaghai wa kikoloni unaoendeleza maendeleo ya ubepari'.

Mapambano haya katika ulimwengu wa kusini yanaakisi wale waliopo Warangal, ambapo CPI(M) kinaongoza maelfu ya watu kupata makaazi, walifaulu kupata nyumba 50,000 mwaka 2008 na kuendelea kupambana kupata nyumba za kutosha mpaka leo.



Nyumba chache miongoni mwa nyumba na mahema 10,000 katika eneo lililotwaliwa,25 Mei,2022.

Hamu ya kulivuka janga la nyumba la kiulimwengu inasambaa . Watu wa Berlin -takribani wakaazi milioni 3.6 – waliandaa kura ya maoni mwaka 2021 juu ya ongezeko la uwezekano wa kutopata makaazi katika mji mkuu huo wa Ujerumani. Kura ya Maoni ilitoa wito kwa dola/serikali kununua nyumba toka kwa makampuni yeyote ya nyumba yenye majumba yanayozidi 3000 katika jiji, hali ambayo ingeathiri nyumba za kupanga 243,000 kati ya milioni 1.5. Kura ya maoni ilipita, ingawa bila shuruti -ya utekelezaji (non -binding). Hili -sambamba na kuongezeka kwa ujasiri kwa watu wanaotwaa maeneo yaliyo wazi na kisha kujenga nyumba zao wenyewe -inaonyesha hali mpya katika vuguvugu la kiulimwengu lipiganialo haki ya makaazi. Kuna ongezeko la kiuelewa kuwa suala la nyumba kubidhaishwa na kufanywa mali-fedha(financial property) inayotumiwa na tabaka la mabilionea kwaajil ulangunzi na udalali ama kuukinga utajiri wao dhidi ya kodi. Mguso huu uko wazi miongoni mwa mavuguvugu yanayopambania haki za makaazi kama vile Despejo Zero (Brazil) na Ndifuna Ukwazi (Afrika Kusini), miongoni mwa mavuguvugu makubwa kama vile MST na Abahlali, na miongoni mwa vyama vya sasa kama vile CPI(M) vinavyoratibu vinavyowaratibu watu kuvuka janga la nyumba kwa kutwaa ardhi.




Wanawake,wanakataa kuondoka katika ardhi, wakinyonga majani ya tuniki kuwa kuwa *bidis* baada ya polisi kuvunja vibanda na yao, Juni 20, 2022.

Utwaaji huu wa ardhi umejaa misukosuko na furaha,hatari ya kupigwa na polisi sambamba na tumaini la maisha ya pamoja. Sehemu ya maisha haya ya inawasilishwa katika nyimbo ambazo mara nyingi hutungwa katika makundi na kutolewa na yeyote. Tunamalizia jarida hili kwa wimbo mmoja wa aina hizo wa wa mjumbe mmoja wa kamati ya Jimbo wa kikundi cha utamaduni ndugu Praja Natya Modali ambaye hutambulika kwa jina Sphoort (likimaanisha 'hamasa') kutoka katika kijitabu kiitwacho *Sphoort Patalu* ('nyimbo za inspiration '):

> Hatutasogea kuondoka hata kwa inchi moja
> Mpaka tupate ardhi kwaajili ya makaazi yetu,
> kibaba ya chakula, na ngwe ya ardhi.
> Tutapambana na wanaotuzuia.
>
> Tuliziinua bendera nyekundu katika ardhi hii,
> tayari kwa pambano la ardhi.
>
> Kiota cha ndege katika matawi.
> Wadudu wana maskani katika majani.
> Sie, tuliozaliwa watu,
> wenye kiu ya kuwa na dari yetu wenyewe,
> ya kuwa na ngwe ya ardhi kwaajili ya makaazi.
>
> Kuhamahama eneo hili mpaka lingine

huku tukihamisha na vibanda,
aibu ya kutokuwepo anuani katika majina yetu.
Kama majani yapeperushwayo na upepo mkubwa,
katika maumivu ya kutokuwa na mahala tunapopaita kwetu.

Mabosi wenye kustawi
Wanaiba maelfu ya ekari
kwa majina ya watoto wao, ndege,na wanyama.
Ila kwa ngwe ndogo ya niombacho,
napigwa viboko nusura ya kifo.

Enyi, mlokuja kutuomba kura:
Tunataka chakula na malazi.
Tupo tayari kwa mapambano mpaka tutakapoyapata hayo.
Tunawathubutu nyie kutuzuia.

Tunamshukuru Jagadish Kumar, mjumbe wa kamati kuu ya CPI(M) ya jimbo na mjumbe wa kamati ya mapambano ya Jakkalodi, kwa kukusanya picha zilizotumiwa katika Jarida hili.

Kwa huba,

Vijay

*Jarida limetafsiriwa katika lugha ya Kiswahili na;* Muhemsi C. Mwakihwelo.